JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

AnwaniyaSimu:"UCHUNGUZI"
SimuNambari: 262323315
Nukushi: 26232332
BaruaPepe: dgeneral@pccb.go.tz
Tovuti: www.pccb.go.tz
Unapojibutafadhalitaja:

Mtaa wa Jamhuri,
S. L. P 1291,
41101 DODOMA,
TANZANIA.

TAARIFA KWA UMMA

IMETOLEWA JIJINI ARUSHA
NOVEMBA 27, 2020

TAKUKURU YATEKELEZA AHADI NA MAELEKEZO YA MHE. RAIS ALIYOAHIDI WAKATI WA KAMPENI ZA KUGOMBEA KITI CHA U-RAIS

Ndugu Waandishi wa Habari,

Tumewaita mahali hapa, ili kupitia kwenu tufanye mrejesho wa ushughulikiaji wa kero mbalimbali za wananchi ambazo Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli – Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jemedari wetu Mkuu, aliahidi katika kampeni zake za kugombea nafasi ya U–Rais nchi nzima, ambapo kwa hapa Arusha **aliahidi yafuatayo:**

Kwanza: Ni Kushughulikia kero mbalimbali zinazowakabili wananchi kwa mfano:

- Wakulima ambao wameshindwa kulipwa fedha zao na Vyama vya Ushirika baada ya kuuza mazao yao kwenye vyama hivyo; **na**

Pili: Ni kero ya kunyanyaswa wananchi wanyonge na watu wenye uwezo kifedha na pengine madaraka – kwa mfano:

- Wananchi kunyang'anywa nyumba, mashamba au mali nyingine kama magari na kadhalika.

Ndugu Waandishi wa Habari,

Kwa kuwa leo tuko jijini Arusha nitaeleza **matukio mawili** yafuatayo ambayo Mhe. Rais aliyatamka wakati alipokuwa katika kampeni zake za kugombea nafasi ya U–Rais akiwa katika mkoa huu:-

Kwanza, ni malalamiko ya ubadhirifu pamoja na ukiukwaji wa Sheria na taratibu za manunuzi katika utekelezaji wa Mradi wa Ujenzi wa Ofisi za Kanda za Mamlaka ya Maji - jiji la Arusha (AUWSA) wenye thamani ya **shilingi Bilioni Tano , Milioni Mia Tatu na Kumi, Laki Nane Ishirini na Tatu Elfu na Mia Mbili Kumi na Tatu (Sh. 5,310,823,213).**

TAKUKURU tayari imeshughulikia kero hii na uchunguzi dhidi ya tuhuma hii upo katika hatua za mwisho.

WITO:

Kupitia hadhira hii tunatoa WITO kwa wale wote wanaohusika katika usimamizi wa michakato ya manunuzi kuhakikisha kwamba wanazingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Manunuzi ikiwa ni pamoja na **MWONGOZO WA UZUIAJI RUSHWA KATIKA MANUNUZI** ambao tuliuzindua Juzi – Novemba 24, 2020 jijini Dodoma.

Uchunguzi kuhusiana na tuhuma hii umethibitisha uwepo wa ukiukwaji wa taratibu za manunuzi hivyo taratibu za kisheria zinaandaliwa.

Kero ya Pili ni, Mgogoro uliohusisha wakulima 83 waliokuwa wakulima kwenye eneo la **Mashamba ya Malula** kwa upande mmoja na Bi. Safia Ahmed Okash kwa upande mwingine, ambao kwa pamoja walikuwa wakigombea umiliki wa eneo lenye ukubwa wa **ekari 2,456** lililopo katika mashamba hayo.

Uchunguzi wa TAKUKURU umeweza kubaini kwamba eneo hilo si la Wakulima hao wala si la Bi. Safia Ahmed Okash, bali eneo hilo ni mali ya Serikali (Halmashauri ya Wilaya ya Meru) ambalo limetengwa na Serikali kwa ajili ya **Mradi wa Malula Industrial**

Park. Walalamikaji wa pande zote mbili wamejulishwa na hivyo kutatua mgogoro husika.

WITO:
Tunatoa WITO kwa jamii kuhakikisha kuwa wanatambua taratibu zote a umulikishwaji wa ardhi ili kuepuka kujiingiza katika migogoro ya aina hii.

Ndugu Waandishi wa Habari,

Kero hizi na nyingine zote zinaendelea kushughulikiwa kwa kasi kubwa katika ofisi zote za TAKUKURU zilizopo katika kila mkoa na kila wilaya hapa nchini na leo hii, **mtashuhudia urejeshwaji wa mali zifuatazo ambazo zipo hapa mbele yenu:**

1. Fedha taslimu kiasi cha Shilingi **Milioni Mia mbili Tisini na Nne, Laki Tano Arobaini na Mbili Elfu Mia Nane Kumi na Tano tu (Sh.294,542,815/-**
   Fedha hizi ni marejesho ya madeni ya Vyama vya Ushirika na pia madai binafsi ya wanyonge yaliyotokana na dhuluma na utapeli uliokuwa umefanywa na waajiri wao; Wengine ni kupitia wakopeshaji umiza pamoja na wabia wa biashara ambao waliingia nao makubaliano yaliyowakandamiza.

2. Leo hii pia nitakabidhi **Hati ya Nyumba moja** ya Bi. Anna Kemilembe - yenye thamani ya zaidi ya shilingi **Milioni Mia Moja** (Sh.100, 000,000/=).

- Nyumba hii ipo jijini Arusha na ilikuwa imechukuliwa na wakopeshaji wa mikopo umiza, baada ya mmiliki wa nyumba hii kukopa fedha kiasi cha Shilingi **Milioni Ishirini na Saba na Laki Tano** (Sh.27, 500,000/-) mwaka 2017 na kuwekewa riba kubwa.

3. Vilevile nitakabidhi **Magari matatu mnayoyaona mbele yenu:**
   - **La kwanza ni Mitsubish Fusso** lenye thamani ya shilingi **milioni 40 pamoja na**

   - **Toyota Corona** lenye thamani ya **shilingi milioni 4**

   Magari haya yote mawili ni mali ya Hidaya Hamad Ally, ambayo yalichukuliwa kinyume na utaratibu na **Bw. Otto Antony Makala** ambaye alimtapeli Hidaya **kwa wizi wa kuaminiwa** kwa kuyabadili umiliki wake na kuyauza bila mwenye mali kushirikishwa.

   Uchunguzi wa TAKUKURU ilifanikisha upatikanaji wa magari hayo ambayo ni mali ya Hidaya kama ilivyoamuliwa na mahakama na leo hii tunayarejesha magari haya kwa Hidaya.

   - Lingine ni Gari aina ya **Toyota Landcruiser** lenye thamani ya **shilingi milioni 45,** mali ya Kampuni ya Tanzanite One.

     Gari hili lilitakiwa kuuzwa kwa mnada na kulipa madai ya mfanyakazi **Salum Mohamed Ally** aliyeachishwa kazi na Kampuni hiyo bila ya kufuata utaratibu.

TAKUKURU imefanikisha upatikanaji wa gari hili kama ilivyoamuliwa na Mahakama na leo hii litakabidhiwa kwa mhusika.

Ndugu Waandishi wa Habari,
Zoezi la ufuatiliaji na urejeshwaji wa mali za wanyonge ni endelevu ambalo linafanyika nchi nzima kwa mujibu wa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11 ya Mwaka 2007 na pia ni sehemu ya utekelezaji wa **ahadi na maelekezo** yaliyotolewa na Jemedari wetu - Mhe. Dkt John Pombe Joseph Magufuli – Rais wa Awamu ya Tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ajili ya kuwatetea wanyonge.

Ninatoa pongezi kwa mkoa huu wa Arusha kwani katika kipindi cha **miezi sita** (Juni 2020 hadi Novemba 2020), wamefanikisha ulipwaji wa kodi ya Serikali iliyokuwa imekwepwa pamoja na urejeshwaji wa madeni na mali, zinazofikia jumla ya shilingi **Bilioni sita, milioni mia nne sabini na sita, elfu sabini na tano, mia tano tisini na tisa tu** (**Sh. 6,476,075,599/-**). Hii ni kasi nzuri inayopaswa kuendelezwa.

Ndugu Waandishi wa Habari,

Natoa **WITO** kwa jamii na wadau wetu wote kuendelea kutuletea taarifa za wanaojihusisha na vitendo vya Rushwa ikiwa ni pamoja na kudhulumiwa, kutapeliwa na kunyimwa haki zao. TAKUKURU tutazipokea na tutazifanyia kazi ili wahusika katika ubadhirifu waweze kuchukuliwa hatua stahiki.

Ninarudia kutoa wito kwa wale wote wanaofahamu kwamba walichukua fedha za umma kwa njia za rushwa, udanganyifu au dhuluma kwa wanyonge, kwamba wanatakiwa wazirejeshe kabla RUNGU LA TAKUKURU halijawafikia.

Ahsanteni sana kwa kunisikiliza na sasa nipo tayari kukabidhi fedha na mali kwa wahusika.

IMETOLEWA NA:

J.J. MBUNGO, *ndc*
BRIGEDIA JENERALI
MKURUGENZI MKUU WA TAKUKURU